BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Pili – Tarehe 16 Februari, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Uchumi ya mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

169. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kumekuwepo na ukiukwaji mkubwa wa Sheria za Barabarani, hali inayopelekea vurugu kubwa na kukosekana usalama katika barabara zetu. Muda mwengine utaona hata gari za Serikali, za Polisi, za Vikosi vya SMZ pamoja na za Mawaziri, zinashindwa kufuata Sheria hizo ikiwa ni pamoja na kutofuata taa za kuongozea gari barabarani, wakati wao ndio kigezo kizuri kwa wengine.

(a) Je, ni hatua zipi madhubuti ambazo Serikali inazozichukua ili kudhibiti hali hii.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa askari wa barabarani wanaachiwa kufanya kazi zao kwa uhuru bila ya kuingiliwa katika kutekeleza majukumu yao.

<u>**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**</u>

88. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Tunaipongeza Serikali yetu kwa kuzingatia haki za watu wenye mahitaji maalum nchini mwetu kwa kuwawezesha kuishi kama watu wengine na kuendelea kuwajengea mazingira mbali mbali rafiki.

(a) Je, kuna watu wangapi wenye mahitaji maalum wasiotembea na kati ya hao wanaosoma wangapi na wasiosoma ni wangapi.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia maisha yao, watu wenye mahitaji maalum wasiotembea.

<u>**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**</u>

49. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Serikali imekuwa ikitilia mkazo kwenye mafunzo ya Amali, Sayansi na Teknolojia, TEHAMA na mafunzo mengine endelevu, ili kumuwezesha mwananchi kujiajiri na kujikomboa kiuchumi. Hata hivyo, hakuna mkakati maalum wa kumuendeleza mwanamke katika mafunzo hayo:

(a) Je, tokea kuanzishwa vyuo vya mafunzo ya amali, Serikali imewapa mafunzo na kuhitimu wanawake wangapi na ni wangapi wameweza kujiajiri na kujikomboa kiuchumi.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa karibuni wa kisera utakaowasaidia wajasiriamali na wafanyabiashara wanawake kupata huduma za ushauri na mafunzo, ili kuongeza uzalishaji na kuweza kuingia katika soko la kiushindani.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

89. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Tunaushukuru Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kwa kuwafundisha wafanyakazi juu ya kujiwekea akiba zao na kufaidika nazo baada ya kumaliza utumishi wao katika Taasisi mbali mbali wanazozifanyia kazi.

(a) Je, kuna wafanyakazi wangapi wameweka fedha zao na sasa hawana kazi na hawakulipwa fedha zao kwa sababu hawajafikia umri uliowekwa na Mfuko huo.

(b) Je, Mfuko huo unawafahamu wafanyakazi waliohai na waliokufa ambao hivi sasa tayari wameshaachishwa ama kuacha kazi na ambao waliweka akiba zao katika Mfuko huo.

(c) Je, ni wafanyakazi wangapi waliokufa, walioacha kazi na wangapi hawajulikani walipo, lakini akiba zao zipo ZSSF.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

36. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembe Samaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Kiembesamaki msingi A na B ni moja kati ya skuli inayosomesha idadi kubwa ya wanafunzi Zanzibar, lakini inakabiliwa na changamoto kubwa za uchakavu wa majengo na miundombinu isiyoendana na uhalisia wa skuli yenyewe sambaba na uchache au uhaba mkubwa wa vitendea kazi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kutatua changamoto hizo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

5. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali kwa kuazimia na hatimae kutekeleza kwa vitendo ujenzi wa barabara mbali mbali za ndani katika maeneo mengi hapa nchini. Pamoja na juhudi na azma hizo, tunafahamu kuwa Serikali kupitia Wizara yako, haitaweza kuzikamilisha

barabara zote kwa wakati mmoja.

(a) Je, ni lini Wizara yako itazifanyia marekebisho angalau kwa kiwango cha kuweka fusi, barabara zote za ndani ambazo hazimo katika utaratibu wa kujengwa kwa kiwango cha lami katika hatua za awali.

(b) Je, ni lini barabara ya Melinne – Makaburini mpaka maguzo ya Kidatu kuelekea Kilima cha Nyarugusu Unguja, itajengwa kwa kiwango cha lami.

(c) Je, ni lini Wizara yako itaijenga kwa kiwango cha lami, barabara ya Msumbiji – Magogoni.

147. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Usafiri wa Baharini kutoka Unguja kwenda Pemba na kurudi umekuwa ni tatizo kubwa kwa kuwa vyombo vilivyopo huchukua muda mrefu baharini na kuna baadhi ya siku safari zao hufika masaa saba (7) kutoka Pemba kuja Unguja au kurudi.

(a) Je, vyombo hivyo ni vibovu au kuchelewa huko kunasababishwa na nini.

(b) Je, Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) hawajaliona hilo.

(c) Je, Serikali kupitia Wizara ina mpango gani na mikakati ipi ya kuondoa usumbufu huo kwa wananchi wa visiwa vyetu viwili.

## Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

15. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kilimo chetu kimevamiwa na tatizo la sumukuvu linaloathiri uzalishaji wa mazao mbali mbali.

(a) Je, ni ipi kauli ya Wizara yako juu ya kuwepo kwa tatizo hili.

(b) Wizara imepiga hatua zipi za mafanikio katika kukabiliana na tatizo hili.

(c) Wizara ina mkakati gani wa dharura na wa muda mrefu

ili kuiondoa kadhia inayodhoofisha uzalishaji hususan kwa wakulima wadogo wadogo.

## Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

112. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Tunaipongeza Serikali kwa kutujengea viwanda vya maji safi na salama ya kunywa, kupitia wawekezaji waliojenga viwanda mbali mbali hapa Zanzibar na hasa wawekezaji wa viwanda viwili vya 'Lulu Pure Drinking Water' na 'Pemba Drinking Water' vilivyopo kisiwani Pemba.

(a) Je, kupitia viwanda hivyo vilivyopo Pemba, ni wafanyakazi wangapi wameajiriwa.

(b) Je, katika idadi hiyo, wazawa wangapi wanaoishi katika maeneo husika wamepata fursa za ajira hizo.

## Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

73. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Inasikitisha kuona kuwa tatizo la utupwaji wa watoto wanaozaliwa katika maeneo mbali mbali ya mji wa Zanzibar linaongezeka, licha ya Idara kutoa taarifa hizo katika vyombo vya habari na kuwataka wananchi waachane na tabia hiyo kwa kuwa watoto hao mara nyingi hukosa huduma kwa wakati na kupelekea vifo vyao.

(a) Kwa nini Wizara baada ya kuwagundua wanamama wanaojihusisha na uhalifu huo, inakosa kutoa taarifa sahihi ndani ya muda muwafaka.

(b) Ni vikao vingapi vya tathmini vilivyowahi kufanywa juu ya hatua madhubuti za udhibiti wa tatizo hilo.

(c) Je, ni lini Serikali itafungua vituo maalum vya kuwahifadhi na kuwalea watoto wanaotupwa na kuwaomba wale wote wasiowataka watoto wao kuwapeleka vituoni humo, bila ya kulazimishwa kutoa taarifa zao.

## Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

45. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ufanisi wa Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa kiasi kikubwa umekuwa ukizoroteshwa na miuundo ya kiutumishi ya mashirika hayo na kutokuwa na nyenzo na uhuru wa kutosha wa kufanya kazi kibiashara.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha kwamba ZECO na ZAWA zinapata uhuru wa kutosha wa kujiendesha kibiashara.

(b) Je, mkwamo wa muundo wa utumishi wa ZECO uliosubiriwa kwa muda mrefu kutoka Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora utakwamukaje.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

144. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kuja na Sera ya Uchumi wa Buluu ambayo vijana wengi wa jimbo la Dimani katika shehia ya Nyamanzi, wameitikia vizuri na kwa vitendo sera hiyo kwa kuanzisha mabwawa ya ufugaji wa samaki wao wenyewe. Hata hivyo, vijana hao wanakabiliwa na changamoto mbali mbali ambazo zinahitaji msukumo wa Wizara ili waendelee na mradi wao wa ufugaji wa samaki.

(a) Je, Wizara itawasaidia vipi vijana hao katika kuunga mkono juhudi zao na kuwatatulia changamoto zinazowakabili kama vile vifaa, mitaji na utaalamu.

(b) Je, ni lini Wizara itawatembelea vijana hao na kusikiliza changamoto zinazowakabili ili kuchukua hatua za kuwasaidia.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Uchumi ya mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**16 Februari, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**